KIJARIDA KUHUSU

# TARATIBU ZA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI

*Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai [1985]*

***The Criminal Procedure Act [1985]***

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

# TARATIBU ZA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI

*Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai [1985]*

***The Criminal Procedure Act [1985]***

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

**SHUKRANI** .......... **5**
**DIBAJI** .......... **6**
**UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU** .......... **8**
**MAONO** .......... **8**
**TAMKO LA LENGO MAHUSUSI** .......... **9**
**LENGO KUU** .......... **9**
**1. Utangulizi** .......... **10**
1.1.Maana ya Jinai .......... 10
**2. Sheria za Jinai** .......... **11**
**3. Matokeo ya Kutenda Kosa la Jinai** .......... **12**
3.1.Kukamatwa (kwa mujibu wa Kifungu cha 11 – 33 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai) .......... 13
3.2.Dhamana .......... 16
3.3.Muda wa kufikishwa mbele ya Sheria .......... 17
3.4.Hati ya Mashtaka .......... 17
**4. Upekuzi na Ukamataji Mali na Vithibitisho au Vielelezo** .......... **18**
**5. Uendeshwaji wa Mashitaka** .......... **27**
5.1.Kukubali Kosa .......... 28
5.2.Kukana Kosa .......... 28
**6. Kusikilizwa kwa Shitaka** .......... **29**
**7. Hukumu** .......... **31**

# SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususani, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Ms. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inaababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako upata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# 1. UTANGULIZI

Mfumo wa jinai unaongozwa na taratibu, kanuni na sheria mbalimbali zilizowekwa na kukubalika katika jamii fulani zitumike kuingoza jamii hiyo. Taratibu, kanuni na sheria hizi zimeweka makatazo mbalimbali ambayo yakikiukwa hutengeneza kosa lijulikanalo kama jinai. Hivyo, kosa lolote linalohatarisha usalama wa raia na mali zao; usalama wa mali na mamlaka za umma; amani na utulivi wa nchi; n.k. na kutamkwa bayana katika sheria, kanuni au taratibu husika, hubainishwa na kuweka adhabu dhidi ya mkosaji.

## 1.1. Maana ya Jinai

Jinai ni kosa au makosa yanayofanywa na mtu/watu; au taasisi kupitia watendaji wake, kinyume cha sheria au taratibu zilizoainisha makosa mbalimbali. Kwa mfano, makosa yote yaliyoainishwa katika Sheria ya Kanuni za Adhabu, (the Penal Code), Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania.

## 2. SHERIA ZA JINAI

Nchi nyingi zilizopo katika Jumuiya ya Madola, makosa mengi ya jinai yameorodheshwa katika sheria ya Sheria ya Kanuni za Adhabu. Pamoja na Sheria ya Kanuni za Adhabu, kuna sheria na taratibu nyingine zimebainisha makosa ya jinai kulingana na utaratibu uliowekwa na jamii/ nchi husika. Sheria nyingine zinazotumika katika makosa ya Jinai hapa Tanzania, ni pamoja na: -

1. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985 (The Criminal Procedure Act);
2. Sheria ya Mahakama za Mahakimu, 1984 (The Magistrates Courts Act);
3. Kanuni za Mwenendo wa Makosa ya Jinai katika Mahakama za Mwanzo (The Primary Court Criminal Procedure Code, 3rd Schedule to CPA);
4. Sheria ya Uhujumu Uchumi (The Economic & Organized Criminal Acts, 1983);

5. Kiwango cha Chini cha Adhabu 1972 (The Minimum Sentence Act);
6. Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 (The Sexual Offences] Special Provisions] Act);
7. Na sheria zingine zote zinazotaja makosa ya jinai.

## 3. MATOKEO YA KUTENDA KOSA LA JINAI

Mtu yeyote anayetuhumiwa na kushtakiwa kwa kosa la jinai, inachukuliwa kuwa ameikosea au ametenda kosa dhidi ya Jamhuri. Maana yake ni kwamba mtenda kosa au mtuhumiwa huwa anachukuliwa kuwa ameikosea jamii ya watu waliokubali na kupitisha sheria au taratibu zilizowekwa.

Mara tu mtuhumiwa au mkosaji anapoonekana ametenda kosa la jinai, zifuatazo ni hatua zinazopaswa kufuatwa:-

### 3.1. Kukamatwa (kwa mujibu wa Kifungu cha 11 – 33 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai)

Hii ni hatua ya kumtia mtuhumiwa nguvuni au chini ya ulinzi kabla ya kumfikisha katika vyombo vya dola. Vyombo vya dola ni pamoja na polisi au mlinzi wa amani.

a. Watu/vyombo vyenye mamlaka ya kukamata mtuhumiwa: Ili kuhakikisha kuwa mtuhumiwa anatiwa nguvuni, vyombo vifuatavyo vimepewa mamlaka ya ukamataji:-
   i. Polisi;
   ii. Afisa Usalama au Askari Kanzu;
   iii. Mtendaji yeyote katika Serikali za Mitaa;
   iv. Mgambo na Sungusungu
   v. Mkuu wa Mkoa;
   vi. Waziri;
   vii. Raia;
   viii. Hakimu;
   ix. Rais wa Nchi.

b. Hatua za ukamataji:

Ukamataji uko wa aina kuu mbili:-

i. Ukamataji wa kutumia hati (warrant of arrest);
ii. Ukamatji bila hati (without warrant of arrest).

» Ukamati wa Kutumia Hati (Warrant of Arrest)

Kwa kawaida hati hii hutolewa na Polisi/ Mahakama kwa ajili ya kumkamata mtu anayetuhumiwa kwa kosa la jinai baada ya Polisi/Mahakama kupata taarifa kutoka kwa mlalamikaji.

Yaliyomo katika hati ya kukamatwa (kwa mujibu wa Kifungu cha 112, cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai):

Hati ya kukamata inapaswa iwe na vitu vifuavyo:-

i. Iwe imetolewa na Hakimu/Jaji;
ii. Lazima iwe na muhuri wa Mahakama;
iii. Iwe imesainiwa;
iv. Lazima iwe na maelezo ya mtuhumiwa k.m. Jina, kabila, dini, n.k.
v. Lazima iseme kuwa mtuhumiwa akamatwe na afikishwe kwenye vyombo vya sheria.

» Ukamataji bila Kuwa na Hati

Watu waliotajwa katika vipengele tajwa hapo juu, wanaweza kumkamata mtuhumiwa bila kuwa na hati ya ukamataji baada ya mtuhumiwa kuonekana ametenda kosa la jinai mbele yao, (kwa mujibu wa Kifungu cha 14, cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai).

## 3.2. Dhamana

Dhamana ni ruhusa anayopewa mtuhumiwa au mshitakiwa wakati akisubiri shitaka lake kupelekwa au kusikilizwa Mahakamani au akisubiri hatma ya rufaa yake. (Angalizo: angalia kitabu chetu cha Haki ya Dhamana kwa ufafanuzi zaidi kuhusu dhana hii ya dhamana).

Dhamana huweza kutolewa na:-

i. Jaji au Hakimu;
ii. Mkuu wa Kituo cha Polisi.

Kwa hiyo mara mtuhumiwa anapofikishwa kituo cha polisi au mahakamani ana haki ya kuomba na kupewa dhamana isipokuwa kwa makosa ya mauaji, uvunjaji wa kutumia silaha, uhaini na makosa ya uhujumu uchumi.

### 3.3. Muda wa kufikishwa mbele ya Sheria

Kwa mujibu wa sheria, mtuhumiwa anapokamatwa na kufikishwa katika Kituo cha Polisi ni wajibu wa Polisi kumfikisha au kupeleka shitaka lake Mahakamani ndani ya masaa 48.

### 3.4. Hati ya Mashtaka

Hii ni hati inayoelezea mambo yafuatayo:-

i. Jina, umri, dini, kabila au taifa na sehemu anayoishi mtuhumiwa;
ii. Kosa au makosa anayotuhumiwa;
iii. Kifungu au vifungu vya sheria alivyovivunja;
iv. Maelezo ya mazingira aliyotenda kosa.

**Angalizo:**
Mwendesha mashtaka anayo ruhusa ya kubadilisha hati ya mashtaka kabla kesi haijaanza kusikilizwa.

## 4. UPEKUZI NA UKAMATAJI MALI NA VITHIBITISHO AU VIELELEZO

a. Upekuzi

Mtuhumiwa anapotiwa nguvuni na kufikishwa Kituo cha Polisi, Polisi hulazimika kufanya upekuzi kwa mtuhumiwa ili kupata vielelezo au vithibitisho. Kazi hii hufanyika kwa mtuhumiwa mwenyewe mara tu anapofikishwa Kituo cha Polisi. Hata hivyo, Polisi wanaweze kulazimika kupata vielelezo zaidi kwenye maeneo mbalimbali yanayohisiwa kuwa mtuhumiwa anaweza kuwa amehifadhi vielelezo au vithibitisho. Polisi wana mamlaka ya kumpekua mtuhumiwa

anapofikishwa Kituo cha Polisi bila kuwa na hati ya upekuzi (search warrant). Lakini Polisi wanapolazimika kupata ushahidi maeneo mengine yanayohisiwa kuwa na ushahidi, wanawajibika kupata hati ya upekuzi. Hati hii hutolewa na Mkuu wa Kituo chochote cha Polisi au Hakimu/Jaji.

b. Muda wa Kufanya Upekuzi

Kwa kawaida upekuzi unapaswa kufanywa siku yoyote (ikiwemo siku ya Jumapili), na unaweza kufanyika masaa yoyote kuanzia jua linapochomoza na kabla ya jua kuzama.

Hata hivyo, polisi wanaweza kuomba kibali kutoka Mahakamani cha kufanyaupekuzi muda wowote.

Endapo imelazimika upekuzi kufanyika wakati wa usiku, Afisa yeyote wa Polisi aliyefanya upekuzi kwa mujibu wa hati ya upekuzi atalazimika kutoa sababu za kufanya hivyo na kutoa taarifa ya upekuzi mbele ya Hakimu.

c. Ukamataji wa Mali na Vielelezo au Vithibitisho

Wakati upekuzi unafanyika, wapekuzi wakiona kitu chochote kinachoweza kuwa ushahidi au kusaidia kama kielelezo katika shitaka au kinachoshukiwa kuwa kimetumika au kingetumika kutenda kosa, basi wakaguzi hao wanaweza kukikamata au kukikuchukua kwa ajili ya ushahidi.

Vielelezo au vithibitisho au mali inapokuwa imechukuliwa ni wajibu wa Polisi kutoa stakabadhi ambayo itakuwa na saini ya mmliki wa vielelezo au vithibitisho au mali iliyochukuliwa au vielelezo vitatumika kama ushahidi Mahakamani.

d. **Uchunguzi wa Kosa**

Baada ya Polisi kumkamata mtuhumiwa, hulazimika kufanya uchunguzi ili kupata ukweli au maelezo yatakayosaidia kupata ukweli wa jambo au mambo yatayosaidia kuendesha shitaka kwa mujibu wa sheria. Katika kufanya hivyo, Polisi hulazimika kufanya na kuzingatia mambo yafuayo:-

e. **Kumhoji Mtuhumiwa**

Maofisa wa Polisi wana uwezo kisheria, kumhoji mtuhumiwa ili kupata taarifa zitakazo saidia uendeshaji wa shitaka. Na kwa upande wa pili, mtuhumiwa naye anayo nafasi ya kujibu mahojiano ya Polisi.

Wakati wa mahojiano, Polisi anapaswa kuyaweka katika maandishi mahojiano yake na mtuhumiwa. Mahojiano haya yanapaswa kufanyika ndani ya saa 24 tangu mtuhumiwa akamatwe.

f. Wajibu wa Polisi Wakati wa Mahojiano

Polisi ana wajibu ufuatao wakati wa mahojiano:-

i. Kumtaarifu mtuhumiwa kuwa ana haki ya kukataa kutoa maelezo yoyote (Kifungu (2));
ii. Kumtaarifu mtuhumiwa jina lake, cheo chake, kosa la mtuhumiwa na kuwa maelezo yake yatatumiwa kama ushahidi wakati wa kuendesha shitaka;
iii. Anapaswa ampatie mtuhumiwa nakala ya maelezo ya mahojiano ili asome na kuyakubali/kuyakataa kuwa ni maelezo sahihi aliyoyatoa ama la;

iv. Anapaswa kumweleza mtuhumiuwa kuwa ana haki ya kupata mwanasheria, na vilevile kuonana na familia yake;
v. Anapaswa kumweleza mtuhumiwa kuwa ana haki ya kupata matibabu kama mtuhumiwa atakuwa anaumwa au ana majeraha;
vi. Kama mtuhumiwa atakuwa ni mtoto wa umri chini ya miaka 16, basi mzazi au mlezi anapswa awepo wakati wa kuuliza maswali;
vii. Polisi anaweza kuongeza muda wa mahojiano, kwa muda usiozidi saa 8. Ikiwa muda wa kawaida na ule wa nyongeza umemalizika, na bado Polisi wanaona kuna haja ya kuendelea na mahojiano, basi, Polisi watalazimika kupeleka maombi Mahakamani kwa ajili ya kuongezewa muda zaidi;

viii. Anawajibu wa kutotumia nguvu wakati wa mahojiano.

g. Wajibu wa Mtuhumiwa Wakati wa Mahojiano:

Mtuhumiwa ana wajibu ufuatao katika mahojiano:

i. Kusikiliza mahojiano dhidi yake na polisi na kisha kujibu au kunyamaza kimya;
ii. Ana haki ya kuuliza jina na cheo cha polisi anayeendesha mahojiano;
iii. Kusoma nakala ya mahojiano na kuikubali/kuikataa kuwa ni sahihi au la kisha kuweka saini kama ni sahihi kuidhinisha kukubali kwake, na ama kutotia saini ili kupinga utofauti wa maelezo yake na yale yaliyopo katika maandishi.

h. Hatua za Kumfikisha Mtuhumiwa Mahakamani (kwa mujibu wa Kifungu 100 – 109)

Baada ya shitaka kufikishwa Mahakamani, Mahakama hutoa wito/ samansi (summons) wa kumuita mtuhumiwa Mahakamani. Wito huo unapaswa uwe:

Umetiwa saini na kugongwa muhuri wa Mahakama. Samasi hupelekwa kwa mtuhumiwa na Polisi, Karani wa Mahakama au mtunishi yeyote atakayepewa amri ya kufanya hivyo na Mahakama.

Mtuhumiwa au mtu yeyote anayepokea nakala hiyo (Samansi) anapaswa kusaini nyuma ya nakala hiyo.

Kama mtuhumiwa hakupatikana, basi samansi atapewa mtu yeyote wa familia au mwajiri wake au mtu yeyote aliye karibu naye. Mtu huyo atalazimika

kutia saini yake nyuma ya nakala. Kama mtuhumiwa ni afisa mkubwa wa serikali au shirika, basi nakala hiyo itapelekwa kwa mkuu wa idara yake na mkuu wake atahakikisha mtuhumiwa anapata nakala ya samansi hiyo.

Kama mtuhumiwa ni Shirika lenye nguvu ya kisheria, basi samansi hiyo itapelekwa kwa viongozi au katibu wa shirika husika. Kama mtu aliye karibu na mtuhumiwa, naye hapatikani, basi Mahakama itatoa ruhusa ya kupeleka nakala hiyo mahali popote anapoweza kupatikana (mbao za Mahakama, kwenye magazeti, n.k). Hivyo basi, mtu aliyepeleka nakala hiyo hulazimika kula kiapo mbele ya Mahakama kuwa amefikisha nakala nakala hiyo.

Baada ya hatua ya kumpelekea samansi kukamilika Mahakama inamtegemea mtuhumiwa kuwepo Mahakamani.

i. Matokeo ya Kutofika Mahakamani

Iwapo mtuhumiwa hatofika Mahakamani na Mahakama itakapofahamishwa kuwa mtuhumiwa alipelekewa samansi, basi Mahakama itatoa amri ya kukamatwa kwa mtuhumiwa (warrant of arrest).

## 5. UENDESHWAJI WA MASHITAKA

Baada ya mtuhumiwa kufikishwa Mahakamani, atasomewa shitaka. Baada ya kusomewa shitaka, mtuhumiwa ana haki zifuatazo:-

i. Kukubali kosa;
ii. Kukana kosa;
iii. Kunyamaza/kukaa kimya; na/au

iv. Kuifahamisha Mahakama kuwa alikwisha kutumikia kifungo kwa kosa hilo hilo.

### 5.1. Kukubali Kosa

Kama mtuhumiwa atakubali kosa, Mahakama itajiridhisha kuwa mtuhumiwa amekubali kosa akiwa na akili timamu au la. Hivyo, Mahakama haina budi kumtia hatiani mtuhumiwa kwa mujibu wa sheria na kifungu kinachohusika.

### 5.2. Kukana Kosa

Iwapo mtuhumiwa atakana kosa, Mahakama inaweza kuamua kusikiliza au kuahirisha na kupanga tarehe ya kuanza kusikiliza shauri hilo.

Hata hivyo, kabla ya kuahirisha kesi Mahakama itamwelezea mtuhumiwa haki yake ya kupata dhamana endapo hakuwa na dhamana.

Vile vile, Mahakama itaziomba pande zote mbili kuita mashahidi au kupeleka mashahidi wao wakati wa kusikiliza kesi.

## 6. KUSIKILIZWA KWA SHITAKA

Mahakama itaanza kusikiliza shitaka kwa kutoa nafasi ya kwanza upande wa mlalamikaji/walalamikaji (Jamhuri) kueleza shitaka na kutoa ushahidi. Katika hatua hii upande, wa utetezi una haki ya kuhoji mashahidi wa upande wa pili ili kuthibitisha shitaka bila shaka yoyote.

Baada ya mahojiano kutoka upande wa utetezi, Mahakama hutoa nafasi ya mwisho kwa upande wa walalamikaji/mlalamikaji kufafanua hoja zilizokinzana wakati wa mahojiano na upande wa utetezi.

Upande wa utetezi hupewa nafasi ya kutoa utetezi wake na kisha kuhojiwa na upande wa walalamikaji/mlalamikajhi kama ilivyoainishwa hapo juu.

**MUHIMU:**
Katika kusiliza makosa ya jinai, Mahakama ya Mwanzo na Mahakama Kuu zinapaswa kuwa na Wazee wa Baraza.

## 7. HUKUMU

Baada ya pande zote mbili kufunga ushahidi na utetezi, Mahakama huwajibika kutoa Hukumu, Amri na Uamuzi. Matokeo ya uamuzi huashiria kifungo, kutozwa faini au kuachiliwa huru kwa mtuhumiwa.

Kabla ya hukumu kusomwa na kabla mshitakiwa kutamkiwa adhabu, mshitakiwa anayo haki yakuomba apunguziwe adhabu kwa kutoa sababu za msingi mfano uzee, ulemavu, kutegemewa na familia na tabia yake nzuri kwa jamii.

Ndugu msomaji, tunatumaini kuwa mpaka sasa umepata ufahamu wa wa mwenendo wa makosa ya jinasi na taratibu zake. Kwa usaidizi zaidi, unaweza kumwona mwanasheria.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva,
Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*